**KARAGWE DISTRICT COOPERATIVE UNION LIMITED**

Tel/Fax: 028-2227105

P.O. Box 14

Email:ltdkdcu@ yahoo.com

**KARAGWE**

---

**TAREHE: 17/03/2020**

# TANGAZO LA ZABUNI MBALIMBALI MSIMU 2020/2021

Chama kikuu cha ushirika wilaya za Karagwe na Kyerwa (KDCU LTD),Kinawatangazia watoa huduma /bidhaa mbalimbali kuleta maombi ya zabuni kwa ajili ya kutoa huduma /kusambaza bidhaa kwa msimu 2020/2021 kama ilivyobainishwa hapa chini.

1. **Zabuni ya kusafirisha kahawa maganda kutoka vyama vya ushirika vya msingi** vya wilaya za Karagwe na Kyerwa kuileta katika maghala /viwanda vya kukoboa kahawa (mwombaji aoneshe gharama kwa kila kilo moja )

   Ada ya zabuni ni Tshs. 100,000/= kuanzia gari 1 hadi 3, na Tshs. 50,000/= kwa kila gari itakayoongezeka.

2. **Zabuni ya uchapishaji vitabu (kwa sampuli itakayotolewa na ofisi),** orodha na idadi ya vitabu vinavyohitajika inapatikana kwa Afisa Ugavi KDCU LTD , na itatolewa mara baada ya mwombaji kulipa ada ya zabuni.

   Ada ya zabuni ni Tshs. 100,000/=

3. **Zabuni ya kusambaza magunia** ya kutunzia kahawa safi aina ya "*Jute –food grade*", size 41*26 inchi, na gram kati ya 0.8 hadi 0.9 kwa kila gunia.

   Ada ya zabuni ni Tshs. 300,000/=

4. **Zabuni ya kusambaza magunia aina ya vero** (polythene bags), size 80*130 cm na uzito wa gram 120.

   Ada ya zabuni ni Tshs. 200,000/=

5. **Zabuni ya kusambaza vipuri mbalimbali vya kiwanda** Mwombaji aoneshe uzoefu wa kusambaza vipuri katika viwanda na hasa vya kukoboa kahawa.Orodha ya vipuri vinavyohitajika inapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi,na itatolewa baada ya mwombaji kulipa ada ya zabuni.

   Ada ya zabuni ni Tshs. 150,000/=

6. **Zabuni ya kusambaza vifaa mbalimbali vya umeme**
   Mwombaji aoneshe uzoefu wa kusambaza vifaa vya umeme katika viwanda.Orodha ya vifaa vya umeme vinavyohitajika inapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi,na itatolewa baada ya mwombaji kulipa ada ya zabuni.

   Ada ya zabuni ni Tshs. 100,000/=

7. **Zabuni ya kusambaza shajara** (stationeries),orodha ya shajara zinazohitajika inapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi KDCU, na inatolewa mara baada ya mwombaji kulipa ada ya zabuni .

   Ada ya zabuni ni Tsh 100,000/

8. **Zabuni ya kukoboa kahawa kwa wenye viwanda binafsi,** Mwombaji aoneshe gharama ya ukoboaji kwa kilo moja ya kahawa. Uongozi wa KDCU utapenda kujiridhisha na miundombinu ya kiwanda cha mwombaji .

   Ada ya zabuni ni Tshs. 300,000/=

9.**Zabuni ya kurekebisha minzani** ,mwombaje aoneshe gharama kwa kila mzani .

Ada ya zabuni ni Tshs. 50,000/=

KARAGWE DISTRICT CO-OPERATIVE UNION

10.**Zabuni ya kutengeneza /kuchonga mihuri** kwa ajili ya kuandika kwenye magunia ya kahawa safi. Mwombaji aoneshe gharama ya kutengeza /kuchonga muhuri kwa kila herufi moja

Ada ya zabuni ni Tshs. 20,000/=

11. **Zabuni ya usambazaji wa Sare mabalimbali za wafanyakazi**(staff uniform) kwa sampuli itakayotolewa na ofisi. Orodha ya sare pamoja na idadi inapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi KDCU LTD.

Ada ya zabuni ni Tshs. 50,000/=

12. **Zabunii ya matengenezo ya magari ya KDCU.**Mwombaji aoneshe uzoefu wa kutengeneza magari ya taasisi mbalimbali .

Ada ya zabuni ni Tshs. 50,000/=

13.**Zabuni ya huduma ya ulinzi** (security service),kwa maeneo ya ofisi kuu,NMC,Kiwanda cha kamahungu na maeneo mengine kulingana na mahitaji ya KDCU LTD yatakavyokuwa ,

Ada ya zabuni ni Tshs. 100,000/=

14.**Zabuni ya kutoa/kuuza mafuta aina ya *"Petrol na Diesel"*** , kwa magari ya KDCU Ltd kwa utaratibu utakaotolewa na ofisi (KDCU Ltd).Mzabuni atatakiwa kuonesha bei iliyopo kwa sasa kwenye barua ya maombi na **mabadiliko ya bei yatazingatiwa** wakati wa kusaini mkataba.

Ada ya zabuni ni Tshs. 150,000/=

15.**Zabuni ya kuchimba kisima cha maji (Water Well Drilling);** Mwombaji aoneshe (kwenye barua) uzoefu wa kuchimba visima katika maeneo ya wilaya ya Karagwe na Kyerwa. Waombaji wafike katika Ofisi za KDCU Ltd **siku ya tarehe 25/03/2020** kwa ajili ya kuoneshwa maeneo ya kuchimba kisima.

Ada ya zabuni ni Tshs. 120,000/=

KARAGWE ... IVE UNION

## MASHARITI YA ZABUNI

1. Waombaji wa zabuni wenye sifa na uwezo watatakiwa kulipa ada ya zabuni kupitia ***CRDB BANK –KDCU LTD GENERAL A/C NO. 01J1090470100,***na kuwasilisha bank slip katika ofisi ya malipo (cash office) ya KDCU kwa ajili ya kupata stakabadhi.

2. Mwombaji atatakiwa kuwasilisha barua halisi (original)ya maombi ya zabuni anayoomba kwa kuambatanisha nakala halisi ya stakabadhi ya malipo ya ada ya zabuni ,vivuli vya VAT,TIN,leseni ya biashara na vyeti vyote husika vitakavyosaidia kutambulisha uhalali wa mwombaji /kazi yake.

3. Kwa mwombaji wa vifaa vilivyoainishwa kwa neno (sampuli) itabidi afike KDCU LTD,Karagwe ili aone sampuli inayohitajika

4. Kamati ya zabuni haitalazimika kumteua mzabuni aliyeomba kwa bei ndogo,vigezo vilivyowekwa ndivyo vitasaidia kupatikana kwa mzabuni

5. Maombi ya mzabuni yawekwe kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri(seal) na juu ya bahasha iandikwe zabuni inayoombwa mfano ; zabuni ya kurekebisha minzani ,kisha bahasha itumwe kwenye anuani iliyopo hapo chini.

6. Ufunguzi wa maombi ya zabuni utafanyika tarehe 01/04/2020 kuanzia saa 04:00 asubuhi ,katika ofisi za KDCU LTD-Karagwe, ambapo waombaji/wawakilishi wao



KARAGWE DISTRICT ... VE UNION

wanakaribishwa kuhudhuria shughuli ya ufunguzi wa zabuni.

7. Kwa maelezo zaidi waombaji wote wa zabuni wanaweza kupata taarifa zaidi kutoka katika ofisi ya Meneja Mkuu wa KDCU LTD

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:

**MENEJA MKUU,**
**KDCU LTD,**
**S.L.P 14,**
**KARAGWE .**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 01/04/2020 saa 04:00 asubui ,na barua za maombi zidumbukizwe kwenye sanduku la zabuni linalopatikana katika ofisi za KDCU.**

KARAGWE DISTRICT ... UNION